**KAULI YA SERIKALI**

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kanuni namba 49, naomba kutoa kauli ya Serikali kuhusu hali ya chakula na uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2015/2016 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukweli kwamba Wizara ilikuwa inaendelea kujipanga kimya kimya, lakini ilipata pia msukumo kutoa tamko ndani ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Vile vile Bunge lilionyesha kuguswa na suala hili la chakula wakati Wizara ilipokuwa ikijibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku, Mbunge, kuhusu wafanyabiashara kuruhusiwa kuendelea kuuza mazao ya chakula nje ya nchi, lilitokana na swali la msingi namba 2093 lilikuwa limeulizwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Kaliua lililohusu ukaguzi maalum uliofanywa kwenye Vyama vya Ushirika vya Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujiridhisha na hali ya usalama wa chakula nchini, Serikali huwa inafanya tathmini kila mwaka. Mwaka huu Serikali ilifanya tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2015/2016 na upatikanaji wa chakula mwaka 2016/2017. Tathmini inaonesha kuwa Kitaifa, uzalishaji wa chakula utafikia tani 16,172,841 za chakula kwa mlinganisho wa nafaka, yaani *grain equivalent* ambapo tani 9,457,108 ni za mazao ya nafaka na tani 6,715,733 ni za mazao yasiyo ya nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nchi ijitosheleze kwa mahitaji ya chakula kwa mwaka 2016/2017 tunahitaji tani 13,159,326 ambapo tani 8,355,767 ni za mazao ya nafaka na tani 4,803,560 ni za mazao yasiyo ya nafaka. Kulingana na takwimu hizo za upatikanaji wa mahitaji ya chakula, nchi itakuwa na hali ya chakula ya kiwango cha utoshelevu wa ziada kwa asilimia 123, ambapo nafaka ni asilimia 113 na yasiyo nafaka *(non-serials)* ni asilimia 140. Viwango hivi vya ziada kwa mazao yote ya chakula ni tani 3,013,515. Kati ya ziada hii, tani 1,101,241 ni mazao ya nafaka na tani 1,912,174 ni mazao yasiyo ya nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimkoa hali hiyo ya chakula kwa mwaka 2016/2017 inaainishwa kuwa ya ziada katika mikoa 11 kwa viwango vya asilimia kati ya 122 na 222. Utoshelevu katika mikoa 12 kwa viwango vya asilimia kati ya 103 na 118 na uhaba katika mikoa miwili kwa viwango vya asilimia kati ya tatu (3) na 93 ambapo mkoa wenye 3% ni Dar es Salaam ambapo kwa kawaida huwa hawalimi. Aidha, pamoja na hali nzuri ya chakula Kitaifa iliyoelezwa hapo juu, katika mikoa 15 yenye uhaba, zipo Halmashauri 43 zenye uhaba mkubwa wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa mazao ya chakula katika mwaka 2015/2016 ulikuwa pungufu ya upatikanaji katika mwaka huu wa 2016/2017. Katika mwaka 2015/2016, uzalishaji wa chakula ulikuwa tani 15,528,820 *grain equivalent* zikiwemo 8,918,999 za nafaka na tani 6,609,821 za mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji ya chakula katika mwaka 2015/2016 yalikuwa tani 12,946,103 ambapo tani 8,190,573 yalikuwa ni mazao ya nafaka na tani 4,755,530 mazao yasiyo ya nafaka. Hii inaonyesha kulikuwa na ziada ya wastani wa tani 2,582,717 za chakula. Hali ya utoshelevu wa chakula ilikuwa asilimia 120. Jumla ya Halmashauri 69 zilikuwa na hali ya chakula isiyoridhisha katika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya hifadhi ya chakula na mpango wa ununuzi kwa msimu wa 2016/2017, Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(NRFA)* ina uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 246,000 kufikia tarehe 6 Septemba, mwaka huu, 2016. *NRFA* ilikuwa na akiba ya tani 67,506,920 ikijumuisha mahindi, mpunga na mtama. Wakala umepeleka jumla ya shilingi 27,778,815,000/= katika Kanda zake kwa ajili ya kuanza ununuzi wa chakula katika mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2016/2017 Wakala unalenga kununua jumla ya tani 100,000 za nafaka. Aidha, Wakala uliomba nyongeza ya shilingi bilioni 69.5 kwa ajili ya kununua nyongeza ya tani 100,000 za chakula. Hii itawezesha Wakala kununua chakula cha hifadhi chenye jumla ya tani 22,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala umeanza ununuzi tarehe 5 Agosti,2016 kwa kufungua vituo vya ununuzi *(collection centres)* katika Kanda za Makambako, Dodoma na Sumbawanga na baadaye Kanda za Arusha na Songea zikaingia katika ununuzi. Jumla ya tani 30,170.457 za chakula, yaani mahindi zimeshanunuliwa hadi kufikia tarehe 6 Septemba, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda ya Shinyanga bado haijaanza ununuzi. Vile vile Bodi ya Nafaka ya Mazao Mchanganyiko imelenga kununua tani 30,000 za mahindi. Hadi kufikia tarehe 6 Septemba, 2016 Bodi ya Mazao Mchanganyiko imenunua mahindi tani 964 katika Mikoa ya Iringa na Ruvuma kwa kutumia fedha zake za mauzo ya unga na pumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa 2016/2017 inaendelea na mpango wa kuiongezea *NRFA* uwezo wa kuhifadhi katika Kanda zake sita baada ya Serikali ya Tanzania kupata mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Kimarekani milioni 55 kutoka Serikali ya Poland. Kiasi hiki cha fedha kitatumika kujenga vihenge *(Silos)* vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 190,000 na maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, uUwezo wa *NRFA* wa kuhifadhi akiba ya chakula ni tani 246,000 kama nilivyosema kwa sasa na hivyo ongezeko hili

litaifanya kuwa na uwezo wa hifadhi ya chakula wa tani 496,000 kwa wakati mmoja. Wakala upo katika hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilijipa muda wa kujipanga kutoa vibali vya kuuza nje ya nchi mahindi na mchele. Aidha, wauzaji wa mazao mengine aina ya nafaka; mikunde na mizizi wameendelea kupewa vibali vya kuuza nje ya nchi. Lengo la muda huo lilikuwa ni kutoa nafasi kwa Serikali kukamilisha taarifa ya tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2015/2016 na hali ya upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2016/2017. Tathmini ya awali ilifanywa kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Vile vile Wizara ilitaka kupata fursa ya kupitia upya mfumo wa utoaji wa vibali kwa kusafirisha mazao nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ilijitokeza baada ya kuona chakula kingi kikisafirishwa nje bila utaratibu maalum ambapo wafanyabisahara wa nchi jirani walikuwa wananunua vyakula mashambani hata kabla havijavunwa. Aidha, hali ya chakula katika nchi zinazotuzunguka siyo nzuri ambapo kati ya nchi 13 za Ushirikiano wa Kusini Mwa Afrika *(SADCC)* na baadhi ya nchi za Afrika Mashariki zina upungufu wa chakula. Hadi tunaandaa taarifa hii, nchi za Kenya na Zambia zimechukua hatua za kusitisha utoaji wa chakula nje ya nchi *(export)* mahindi na mchele na mazao yanayotokana na nafaka hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii pamoja na kuwa ni fursa kwa wakulima wetu kupata bei nzuri, lakini inaweza kuwa janga kwa Taifa letu kama haitakabiliwa vizuri. Muda huu wa kujipanga usichukuliwe kuwa Wizara inawaingilia wakulima kutumia fursa ya soko, lakini Serikali inayo jukumu la maslahi mapana ya kuhakikisha kuwa nchi haiingii kwenye janga la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kwa Mamlaka yake iliyonayo, inalo jukumu la kuhakikisha wakulima wanafanya kilimo biashara ambapo ni pamoja na kuwatafutia masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa kutoa vibali, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa sasa ndiyo yenye dhamana ya kutoa vibali kwa kuuza na kuingiza mazao ya chakula kwenda na kutoka nje ya nchi. Vile vile Wizara ilikasimu mamlaka ya kutoa vibali kwenye Sekretarieti za Mikoa msimu wa kuanzia 2014/2015. Utaratibu huu ulilenga kusaidia Wizara kujua chakula kinachosafirishwa nje na kuingizwa ndani ya nchi na kuweza kufanya maamuzi ya msingi. Mfumo huu umeonesha upungufu kinyume na matarajio ya Wizara. Baadhi ya upungufu ni huu ufuatao:-

(1) Utaratibu haukuweka kiasi cha juu kinachoruhusiwa na mtoa kibali; na mfano zipo kampuni zilikuwa zinapewa hadi tani 350,000 kwa mara moja

ambapo ni mara mbili ya uwezo wa hifadhi ya *NRFA*. Hii ilikuwa ni kama kuhamisha chakula cha nchi na siyo biashara.

(2) Mfumo haukuwa na uratibu mzuri ambapo mfanyabiashara aliyenyimwa kibali na mamlaka moja aliweza kukipata kutoka mamlaka nyingine bila shida yoyote.

(3) Kiasi kilichosafirishwa nje ya nchi hakikujulikana kwa urahisi kutoka kwenye mamlaka inayohusika kutoa vibali na mambo mengine. Ili kukabiliana na upungufu huo katika muda huu wa kujipanga Wizara imefanya mabadiliko kwa Watendaji ndani ya Wizara na Taasisi zake ili kuleta ufanisi katika utendaji. Vile vile Wizara imekuwa ikifanya majadiliano na Wizara zinazohusu usalama wa chakula, biashara na maafa ili kuweza kuweka mfumo bora wa uratibu na utoaji wa vibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeendelea kupitia sheria, kanuni na miongozo inayosimamia tasnia ya nafaka ili kuona namna bora ya kutoa vibali. Ilifahamika kuwa kwa kutumia Sheria ya Usalama wa Chakula iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2009 ipo fursa ya kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Tasnia ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Hivi sasa Wizara iko katika hatua za mwisho za kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao mchanganyiko (*cereals and other produce regulatory authority)* ambayo kulingana na sheria hiyo itakuwa na mamlaka ya kutoa vibali ikiwa ni pamoja na kudhibiti ubora, viwango na bei za mazao ya aina ya nafaka na mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa muda mfupi wa Wizara ni kuwa vibali vyote vitatolewa Wizarani wakati utaratibu wa kuunda Mamlaka hiyo unakamilishwa. Utaratibu huu uliowekwa unazingatia ufanisi na urahisi wa mawasiliano wa kutuma maombi moja kwa moja Wizarani au kupitia Sekretarieti za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali imeanza maandalizi ya kufanya tathmini ya kina kuhusu hali ya chakula na lishe hapa nchini *(Comprehensive Food and Nutrition Security Vulnerability Assessment)* ikihusisha Halmashauri zenye maeneo yenye uhaba zilizobainishwa katika tathmini ya awali ambazo ni Halmashauri za Mkoa wa Tanga, yaani Halmashauri ya Mkinga, Muheza, Kilindi, Handeni; Handeni *District Council* na Handeni *Town Council,* Korogwe *District Council* na *Town Council* na Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida, ni Halmashauri za Itigi, Manyoni, Iramba na Mkalama. Mkoa wa Mara; Halmashauri za Musoma *District Council,* Rorya na Butiama. Mkoa wa Dodoma; Halmashauri za Chemba, Kongwa na Chamwino. Mkoa wa Manyara; Babati *District Council,* Kiteto na Mbulu. Mkoa wa Arusha; Arusha *District Council* Meru na Monduli. Mkoa wa

Kilimanjaro; Halmashauri ya Hai, Moshi *District Council* na Mwanga. Mkoa wa Morogoro; Morogoro *Municipal Council,* Mvomero, Morogoro *District Council.*

Mkoa wa Pwani; Halmashauri ya Chalinze na Kibaha *District Council.* Mkoa wa Mwanza, Halmashauri ya Magu, Ukerewe, Misungwi na Kwimba. Mkoa wa Njombe; Halmashauri ya Makete na Ludewa. Mkoa wa Lindi; Halmashauri ya Liwale, *Lindi District Council* na Kilwa. Mkoa wa Shinyanga; Halmashauri ya Kishapu. Mkoa wa Iringa; *Iringa District Council* na Mkoa wa Simiyu; Halmashauri ya Busega.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini hii inatarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu na itasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na wadau wengine wa maendeleo ikiwemo *FAO, WFP* na *UNICEF.* Tathmini hii itaiwezesha Serikali kutambua idadi ya watu na kiasi cha chakula kitakachohitajika kwa ajili ya kaya zenye uhaba wa chakula na lishe pamoja na mahitaji mengine kama vile mbegu kwa ajili ya msimu unaofuata na kuchukua hatua mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenendo wa bei za mahindi na mchele. Serikali imekuwa ikiendelea na ufuatiliaji wa mwenendo wa bei za mazao hususan mahindi na mchele ili kujiridhisha na usalama wa chakula na upatikanaji wake. Mwenendo wa bei za mazao haya sokoni kwa kipindi cha mwezi Agosti, 2015 na Agosti, 2016 kutoka kwenye masoko 13 kati ya masoko 25 ya Miji Mikuu hapa nchini umekuwa ukipanda na kushuka kutokana na sababu mbalimbali. Moja ya sababu ni pale kipindi cha mwisho cha msimu hakuna mazao yanayoingia sokoni na hivyo kupelekea bei kupanda na mwanzo wa msimu bei hushuka kutokana na mazao mengi kuingia sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahindi katika kipindi cha Agosti, 2015 bei ya wastani kwa mahindi kwa gunia la uzito wa kilo 100 ilikuwa sh. 58,000.444 ukilinganisha na wastani wa sh. 55.571 kwa kipindi cha Agosti mwaka huu 2016 ampabo imeshuka kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya juu kwa mwezi Agosti kufikia tarehe 31, 2016 ilipatikana katika soko la Moshi Mjini ambapo gunia la kilo 100 liliuzwa kwa sh. 78,437 na bei ya chini ilikuwa ya sh. 39,214 katika soko la Mjini Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa bei ya mchele, takwimu zinaonesha kwamba kwa kipindi kama hiki cha mwezi Agosti mpaka tarehe 31, 2015, bei ya wastani ilikuwa sh. 159,700/= kwa gunia la kilo 100 ikilinganishwa na shilingi 136,276/= kwa gunia la kilo 100 kwa Agosti 31, mwaka huu. Bei ya juu kwa mwezi Agosti kufikia tarehe 31 mwaka huu ilipatikana katika Soko la Songea ambapo gunia la kilo 100 liliuzwa kwa sh. 190,000/= na bei ya chini ilikuwa ni sh. 95,500/= katika soko la Mjini Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwenendo wa bei kama ulivyoelezwa hapo juu, awali kwa ujumla hali ya usalama wa chakula inaridhisha hivyo; kumekuwa na umuhimu wa kuendelea kutafuta masoko ndani na nje ya nchi ili kutoa fursa kwa wazalishaji kujipatia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Kilimo ya mwaka 2013 pamoja na mambo mengine inatambua na kuhimiza kilimo cha kibiashara na Taifa kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sote kufahamu kuwa bei ya vyakula nchini ikipanda huwa na athari mbaya ya jumla kwa uchumi wa nchi yetu kama ilivyo nishati na husababisha thamani ya sarafu yetu kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika kuboresha hali ya usalama wa chakula, kuongeza ari ya wakulima katika uzalishaji wa mazao ya chakula hapa nchini na kujiongezea kipato, Wizara inafanya yafuatayo:-

(1) Wizara inapitia upya mfumo wa utoaji wa vibali vya kusafirisha chakula nje ya nchi ili kuiwezesha kufuatilia kwa ukaribu kuliko ilivyo hivi sasa.

(2) Wizara inafanya tathmini ya kina (*Comprehensive Food and Security Vulnerability Assessment)* kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu katika maeneo yenye uhabawa chakula kama nilivyosema awali.

(3) Kuhimiza wananchi kuhifadhi chakula cha kutosha kwa matumizi katika kaya ikiwa ni pamoja na kuihamasisha sekta binafsi kuendelea kushiriki katika kutoa masoko ya kununua na kuuza mazao katika maeneo yenye uhaba.

(4) Wizara inahimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha vituo vya kununulia mazao, *market centers* ili kuzuia wanunuzi wa nje ya nchi kununua mazao mashambani.

(5) Katika mazingira ya mabadiliko ya tabia ya nchi yanayoikabili dunia ikiwemo upungufu wa mvua, Wizara inaendelea na juhudi zake za kuhimiza na kupanua kilimo cha umwagiliaji mashambani kwa kuimarisha miundombinu iliyopo, kujenga mipya na kuvuna maji ya mvua ili kuongeza uzalishaji kwa tija.

Utabiri wa hali ya hewa uliotolewa na mamlaka ya hali ya hewa nchini *(TMA)* umeonesha kwamba kutakuwa na mvua za wastani na chini ya wastani katika maeneo yenye mvua za vuli jambo ambalo litasababisha mavuno hafifu

katika msimu ujao. Kwa hali hiyo, wananchi wanashauriwa na kuhimizwa kulima mazao yanayostawi kwa muda mfupi na kuhimili ukame.

(6) Wizara inahimiza Sekta binafsi iendelee kujenga maghala na kuhifadhi kama mbinu mbadala na muafaka katika kuhakikisha wakulima hawapotezi mazao yao baada ya kuvuna *(post harvest loses)*.

(7) Wizara inahamasisha na kuelimisha wafanyabiashara kuuza nje ya nchi unga wa mahindi badala ya mahindi au mchele badala ya mpunga ili kuendana na sera ya kuendeleza viwanda hapa nchini na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kusema kuwa Wizara itakamilisha utaratibu mpya wa kuuza chakula nje ya nchi, ndani ya wiki moja kuanzia leo tarehe 9 Septemba, 2016 na vibali kwa aina ya mazao ya mahindi na mchele vitaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutuunga mkono na kuendelea kutupa *support* pale tunapofanya maamuzi haya kwa niaba ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.